JARIDA MAALUMU LA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2023 | HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO



# MAKAMBAKO YETU

*www.makambakotc.go.tz* | *Kitengo cha Mawasiliano Serikalini* | *Jarida Maalumu La Mwenge wa Uhuru 2023*



# MAPOKEZI YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2023 - H/W MJI MAKAMBAKO

JARIDA MAALUMU LA MWENGE 2023.indd 1 5/19/2023 5:25:15 AM

## UTANGULIZI

Mwenge wa Uhuru 2023 katika Halmashauri ya Mji Makambako Ulipokelewa mnamo Aprili 30,2023 katika kijiji cha Mawande,Viwanja vya Shule ya Msingi Mawande Kata ya Utengule,kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

Mwenge wa Uhuru kwa mwaka huu ulitembelea jumla ya Miladi sita yenye thamani ya mil. 745 na kukimbizwa umbali wa kilomita 50.6.

Mei mosi,2023 Mwenge wa Uhuru ulikabidhiwa Mkoa wa Iringa na Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Anthony Mtaka ambapo Kimkoa Mwenge wa Uhuru katika Mkoa wa Njombe ulikimbizwa umbali wa kilomita 517 na kukagua,kutembelea na kuzindua jumla ya miradi ya maendeleo 45 yenye thamani ya Bil. 346.5 katika Halmashauri sita zilizopo Mkoa wa Njombe.








## MWENGE WA UHURU 2023: Wazindua mradi wa ujenzi wa madarasa 2 na ofisi 1 shule ya msingi Mawande

Mwenge wa Uhuru mwaka 2023 umezindua mradi wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi moja katika shule ya Msingi Mawande,iliyopo Kata ya Utengule ambao hadi kukamilika umegharimu jumla ya mil. 49.5 na kupanda miti ya parachichi.

Awali akisoma taarifa ya mradi mbele ya Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa, Mwalimu Mkuu wa shule wa shule ya Msingi Mawande, Mwl. Octavian Mkinga amesema kuwa, mradi huo ulipokea fedha za Ruzuku toka Serikali Kuu Mil. 50 zilizotolewa kwa kwa ajili ya shule kongwe na nguvu za wananchi mil. 3.3 na kuwa na jumla ya mil. 53.3 na hadi kukamilika kwa mradi huo jumla mil. 49.5 zimetumika ikiwa ni pamoja na ununuzi wa madawati ya wanafunzi 50, meza 2 na viti 2 vya walimu.

Amesema kuwa, mradi huu ulianza kutekelezwa rasmi Oktoba 31, 2022 kwa kutumia mfumo wa "force Account" , ambapo vifaa vya ujenzi vilinunuliwa na kusimamiwa na Kamati zinazohusika na usimamizi wa mradi huo ,pamoja na Kamati ya Shule na kwa sasa mradi umekamilika na madarasa yanatumika.

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,Ndg. Abdalla Shaibu Kaim mara baada ya kupokea na kukagua mradi huo,amekiri kuridhishwa na utekelezaji wa mradi huo,na kutoa rai kwa Wahandisi kutumia taaluma zao vizuri katika kipengele cha ununuzi wa vifaa vinavyohitajika kuepuka gharama zisizo na ulazima.

Aidha amesema kuwa, lengo kuu la Serikali kutoa fedha za ujenzi wa madarasa ni kuboresha miundombinu ya Shule ,na kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani na kuwawezesha wanafunzi kusoma vizuri na kuongeza ufaulu kwa kuboresha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji.

Shule ya Msingi Mawande ni moja kati ya Shule 45 za Serikali zilizopo ndani ya Halmashauri ya Mji Makambako, ni miongoni mwa shule kongwe nchini,ambayo ilianzishwa mwaka 1953.



**Katika Picha:** Ni Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,Ndg. Abdalla Shaibu Kaim akikagua moja ya dirisha katika darasa mojawapo kati ya mawili yaliyozinduliwa na Mwenge wa Uhuru 2023. **Kushoto:** Ni Mhandisi wa ujenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako,Mhandisi. Salim wakati wa zoezi la ukaguzi wa mradi huo.




**Katika Picha**: Ni Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,Ndg. Abdalla Shaibu Kaim akipanda mti wa parachichi katika shamba la shule ya Msingi Mawande ili kuboresha lishe ya wananfunzi shuleni.



**MWENGE WA UHURU 2023 :Wakagua muendelezo wa mradi wa uhifadhi na utunzaji wa msitu wa asili shule ya sekondari Mtimbwe na kukabidhi mizinga ya nyuki 20**

Mbio za Mwenge wa Uhuru 2023,mnamo aprili 30,mwaka huu umekagua muendelezo wa Mradi wa Uhifadhi na utunzaji wa msitu wa asili uliopo katika Shule ya sekondari Mtimbwe, ulioanza februari 25,2005 ukiwa na jumla ya ekari 50, na kukabidhi mizinga 20 ya nyuki.

Akisoma taarifa ya mradi huo mbele ya Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Mkuu wa Shule ya sekondari Mtimbwe, Mwl. Zuberi Kilingo amesema kuwa, msitu huo unatumika kama nyenzo ya kufundishia wanafunzi mada zinazohusu misitu ya asili na Kupendezesha mazingira ya shule, kuzuia mmomonyoka wa ardhi na kupata hewa safi katika msitu huo pia wameanzisha ufugaji wa nyuki ambapo wanafunzi wanapata nafasi ya kujifunza namna ya kufuga nyuki ili kujipatia kipato kwa kuuza asali,na shule inanufaika kupitia uuzaji wa asali,fedha zinazopatikana zinatumika kutatua changamoto mbalimbali za shule.

“Tumeanzisha mradi huu wa kufuga nyuki kwa kuanza na mizinga nane ambayo kwa wastani kila mzinga unatoa asali kiasi cha lita kumi ,kwa mizinga yote tumekuwa tukipata kiasi cha Tshs. 800,000 kiasi hiki cha fedha kimekuwa kinasaidia kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabiri Shule yetu lakini pia wanafunzi wanapata ujuzi wa ufugaji nyuki”,alisema Mwl. Kilingo.

Baada ya kusomwa kwa taarifa hiyo ,Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,Ndg.Abdalla Shaibu Kaim alitembelea na kukagua muendelezo wa uhifadhi na utunzaji wa msitu huo, na kukabidhi mizinga 20 kwa wanafunzi wa shule hiyo ili kuongeza uzalishaji wa asali.

Pia,amepongeza jitihada zinazofanyika katika utunzaji wa msitu huo wa asili na mazingira kwa ujumla,na kutoa rai kwa wananchi kuendelea kutunza na kuhifadhi mazingira kwa maslahi mapana ya taifa.

Mradi wa uhifadhi na utunzaji wa mazingira ya msitu huo wa asili ulizinduliwa na Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2016,Ndg. George Jackson Mbijima katika Mbio za Mwenge wa Uhuru Halmashauri ya Mji Makambako mnamo Juni 18,2016.




**MWENGE WA UHURU 2023 : Waweka Jiwe la Msingi mradi wa Ujenzi wa Zahanati ya Ikelu**

Mradi wa ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Ikelu uliogharimu zaidi ya mil. 191 umekaguliwa na kuwekwa jiwe la msingi mnamo aprili 30,mwaka huu na Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Ndg.Abdalla  Shaibu Kaim na kugawa vyandarua 100 kwa kina mama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano ili kujikinga na malaria.

Baada ya kukagua na kuridhishwa kwa utekelezaji wa ujenzi wa zahanati hiyo,Ndg Kaim ameipongeza Halmashauri ya Mji Makambako kwa utekelezaji mzuri wa mradi na kutoa rai kuhakikisha vifaa vinapatikana na huduma zianze kutolewa ,ili dhana ya ujenzi wa zahanati hiyo uwe na tija kwa wananchi kwani fedha za ujenzi wa Zahanati hiyo ni kodi za Watanzania.

Aidha,ametoa rai kwa wananchi kuendelea kujikinga dhidi ya malaria na kufika katika vituo vya afya pindi wanapohisi homa,ili waweze kupimwa na kupata huduma stahiki kwani si kila homa ni malaria ,na kuwataka kina mama wajawazito na wenye watoto chini ya miaka mitano,ambao wamekabidhiwa vyandarua kuvitunza na kuvitumia kwa lengo lililokusudiwa na Serikali kwani vyandarua hivyo vinatokana na kodi za Watanzania.

Awali akisoma taarifa ya mradi huo,Bi. Neema Chaula,Mratibu wa TASAF katika Halmashauri ya Mji Makambako, amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ,Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa fedha zilizotumika katika ujenzi wa Zahanati hiyo kupitia Mradi wa kupunguza umaskini TASAF (OPEC III), kwa kutambua  changamoto ambazo wananchi  wa  Ikelu walizipata kwa kukosa Zahanati ya Serikali.




**MWENGE WA UHURU 2023: Watembelea na kukagua Mradi wa kuongeza uzalishaji na tija wa Shamba la Mahindi kupitia utekelezaji wa mpango wa mbolea za ruzuku msimu wa mwaka 2022/2023**

Mbio za Mwenge wa Uhuru 2023 katika Halmashauri ya Mji Makambako,zimetembelea na kukagua shamba la Mahindi la Bi. Edda Sanga ,mmoja kati ya wakulima 12,714 walionufaika na mbolea za ruzuku,zilizotolewa na Serikali katika msimu wa mwaka 2022/2023.

Bi. Edda Sanga ambaye pia ni Mjasiriamali anayejishughulisha na na kilimo biashara cha mazao mbalimbali yakiwemo Mahindi, Maharage na Parachichi, Kwa msimu wa kilimo wa 2022/2023 amefanikiwa kulima jumla ya ekari 47 za zao la Mahindi ambapo ekari 32 zipo katika Halmashauri ya Mji Makambako na ekari 15 zipo Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe.

Bi. Sanga amesema kuwa,Kupitia namba za siri za mbolea za Ruzuku alipata jumla ya mifuko 133 ya mbolea za aina mbalimbali zenye jumla ya thamani ya zaidi ya Mil.16.2 ambapo kati ya kiasi hicho cha fedha amechangia Mil. 9 na Serikali imegharimia ruzuku yenye thamani ya Mil. 7.2.

Amebainisha kuwa,Katika msimu huu wa kilimo amefanikiwa kuongeza eneo la uzalishaji kutoka ekari 20 alizolima mwaka jana hadi ekari 47, kutokana na kupungua kwa gharama za mbolea na anatarajia kupata jumla ya tani 117.5 sawa na kilo 117,500 za mahindi na kuongeza pato la familia na chakula.

Kwa niaba ya wakulima wengine, ameishukuru Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe, Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweka ruzuku kwenye mbolea ,ambayo imewapunguzia gharama za kununua mbolea na kuwasaidia kuongeza uzalishaji wenye tija na kipato cha Mkulima.

Ndg. Abdalla Shaibu Kaim,Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa amempongeza Bi. Edda Sanga kwa kilimo anachokifanya, ikiwa ni pamoja na kutumia vizuri fursa ya mbolea za ruzuku iliyotolewa na Serikali na kuwataka vijana kuiga mfano kwa mkulima huyo kwani kilimo kinalipa.

Katika Halmashauri ya Mji Makambako jumla ya wakulima 12,714 wamenufaika na mbolea za ruzuku,ambapo wamenunua jumla ya mifuko 61,596 sawa na tani 3,079.8.




## MWENGE WA UHURU 2023: Wazindua klabu ya kupinga rushwa shule ya sekondari Makambako kwa kusaini hati na kuweka jiwe la msingi

Klabu ya kupinga rushwa katika shule ya sekondari ya Makambako, imezinduliwa rasmi april 30,mwaka huu na Mbio za Mwenge wa Uhuru 2023 ikiwa ni moja ya Ujumbe wa kudumu wa Mbio za Mwenge wa kupinga rusha usemao "Kuzuia Rushwa ni jukumu lako na langu; tutimize wajibu wetu" .

Mara baada ya uzinduzi wa klabu hiyo, Ndg. Abdalla Shaibu Kaim,Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa amewapongeza wanafunzi wanaounda klabu hiyo,kwa kujiunga na klabu ya kupinga rushwa ambayo ni adui wa haki na kuwataka kuendelea kuwa wazalendo katika kulinda maslahi yao na wananchi wengine kwa ujumla kwa manufaa ya taifa.

Awali akisoma taarifa ya klabu hiyo Mwanafunzi Minza Lugata,ambaye ni mwenyekiti wa klabu hiyo amekiri kuwa,katika klabu hiyo wanafunzi wanapata nafasi ya kujengwa kimaadili kwa kupata uelewa mkubwa wa elimu ya rushwa ambayo wanaisambaza kwa wanafunzi wengine ambao si wanachama na jamii inayowazunguka.

Amesema wanaklabu ya kupinga Rushwa wanatumia njia mbalimbali kuelimisha Umma ikiwa ni pamoja na semina, maigizo uchoraji wa katuni, utunzi wa mashairi, ngonjera, nyimbo na kufanya midahalo inayokemea vitendo vya rushwa na kushiriki katika shughuli za kijamii.

Klabu ya wapinga rushwa katika Shule ya Sekondari Makambako ilianza rasmi mwaka 2007 na ina wanachama 641 ,Wasichana 505 na Wavulana 136 kwa Lengo la kuwawezesha wanafunzi kushiriki katika Mapambano dhidi ya rushwa, kwa kuzingatia kuwa Wanafunzi ndio watendaji wa kesho hivyo wakijengwa kimaadili ni wazi kuwa Tanzania itakuwa na kizazi kinachozingatia maadili na kisichovumilia hata kidogo vitendo vya rushwa katika jamii.



**MWENGE WA UHURU 2023: Wakagua na Kuweka jiwe la msingi katika jengo la hoteli ya ghorofa tatu**

Mradi wa ujenzi wa Hoteli ya Ghorofa tatu inayomilikiwa na Mfanyabiashara BI.BERNADETHA SANGA,umekaguliwa na kuwekwa jiwe la msingi na mbio za Mwenge wa Uhuru 2023.

Akisoma taarifa ya mradi huo Msimamizi wa Ujenzi wa Mradi huo Mhandisi mshauri, Sansutwa Simtali Ltd amesema kuwa mradi huo ulianza rasmi Mwezi Mei Mwaka 2021 na unategemea kukamilika Mwezi Januari Mwaka 2024 ,jengo hilo la Hoteli likiwa na idadi ya vyumba vya kulala wageni vipatavyo 10.

Ameongeza kuwa, Ujenzi wa Jengo la Hoteli hiyo hadi kukamilika utagharimu mil. 420 ambapo kwa sasa umegharimu jumla ya mil. 380 na baada ya kukamilika kwa Mradi huo umelenga kuboresha huduma ya Malazi ya wageni katika Mji wa Makambako na Mkoa wa Njombe kwa ujumla, Kuboresha maisha ya mwekezaji pamoja na kutoa ajira kwa vijana ambapo mradi ukikamilika utatoa ajira kwa vijana wapatao 20

Mara baada ya ukaguzi wa jengo na nyaraka za ujenzi wa hoteli hiyo, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa Ndg. Abdalla Shaibu Kaim alimpongeza Bi. Bernadetha Sanga ambaye ndiye mmiliki wa jengo hilo kwa kufanya uwekezaji mkubwa,ambao utamuwezesha kuongeza kipato na kutoa huduma bora kwa wakazi na wageni wa Mji wa Makambako na ajira kwa vijana.



## MWENGE WA UHURU 2023: Wapanda miti 500 katika chanzo cha maji cha bwawani

Mbio za Mwenge wa Uhuru 2023 zimefanikisha upandaji wa miti 500 kwenye chanzo cha Maji cha Bwawani ,kilichopo Kati ya Mtaa wa Bwawani,Kata ya Mjimwema na Mtaa wa Uzunguni,Kata ya Maguvani katika Halmashauri ya Mji wa Makambako, ikiwa ni Chanzo kinachotokana na chemichemi za asili zilizopo kwenye eneo hilo chenye ukubwa wa mita za mraba 101,187 kikiwa kimezungukwa na uoto wa asili.

Mhandisi Oscar Lufyagile, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mjini Makambako(MAKUWASA), amesema kuwa MAKUWASA ilipatiwa kibali (RBWB 1687) cha matumizi ya Maji na Bodi ya Maji Bonde la Rufiji ,kwa lengo la kuyavuna na kuyasambaza kwa Wananchi wa Makambako ,kwa ajili ya matumizi mbalimbali ambapo hadi sasa jitihada mbalimbali zimefanyika za kuhakikisha chanzo hicho kinahifadhiwa na kudumu kwa muda mrefu.

Mhandisi Lufyagile amesema kuwa,jitihada zilizofanyika hadi sasa ni pamoja na upandaji wa miti 400 rafiki na vyanzo vya maji ,Ukataji wa miti 75 isiyorafiki na Maji,Uondoaji wa makazi 12 yaliyojengwa ndani ya mita 60 kwa kuvamia chanzo,Uwekaji wa Alama za mipaka kuzunguka chanzo,Uwekaji wa mabango ya kutoa ILANI kwa Wananchi ili wasifanye shughuli za kibinadamu katika maeneo ya chanzo na Ujenzi wa mfereji wa kuzuia Maji machafu ya mvua yasiingie kwenye chanzo pamoja na Utoaji wa elimu ya Uhifadhi wa chanzo na mazingira katika Mitaa inayozunguka chanzo hicho.

Ameongeza kuwa, Jumla ya mil. 77.3 zimetumika katika utekelezaji wa kuhifadhi chanzo hicho kuanzia mwaka 2017 ,na zoezi la uhifadhi ni endelevu hasa upandaji wa miti rafiki na vyanzo pamoja na uondoaji wa miti isiyorafiki na vyanzo ili kuongeza uzalishaji wa maji ambapo tangu uhifadhi wa chanzo hicho ulipoanza hadi sasa Uzalishaji wa maji umeongezeka kutoka lita 249,600 hadi lita 400,000 kwa siku na kupeleke ongezeko la wanufaika wa maji kutoka wananchi 3,328 hadi 5,333 kwa siku.

Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,Ndg. Abdalla Shaibu Kaim amepongeza uhifadhi wa chanzo cha maji cha Bwawani na kutoa shukrani na pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jitihada kubwa anazoendelea kuzifanya hususani kwenye Sekta ya Maji, kwa kuhakikisha anamtua Mama ndoo kichwani na kuwataka wananchi kuendelea kutunza vyanzo vya maji kwa kupanda miti na kutofanya shughuli za kilimo kwenye vyanzo vya maji.

Jumla ya Miti 500 imepandwa na Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa pamoja na timu yake,Viongozi wa Chama na Serikali pamoja na wananchi.



**Katika picha:** Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,Ndg. Abdalla Shaibu Kaimu akikagua mradi wa chanzo cha maji wa Bwawani ,akiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Makambako(MAKUWASA),Mhandisi. Oscar Lufyagile na viongozi wa Chama na Serikali Wilaya ya Njombe.



## MATUKIO YA PICHA

Baadhi ya picha katika eneo la mapokezi ya Mbio za Mwenge wa Uhuru - shule ya msingi Mawande





Madarasa mawili na ofisi moja yaliyofunguliwa na Mwenge wa Uhuru shule ya Msingi Mawande



**MWENGE WA UHURU 2023: Waridhishwa na mradi vijana wa kutengeneza chaki na kuiagiza Halmashauri kutafuta soko la uhakika wa bidhaa hiyo.**

Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,Ndg. Abdalla Shaibu Kaim ameridhishwa na utendaji kazi wa Kikundi cha vijana wajasiriamali Youth Forum, ambacho ni moja kati ya vikundi vilivyonufaika na mkopo wa asilimia 10 unaotolewa na Halmashauri kwa uzalishaji wa bidhaa aina ya chaki na kupata ajira ya uhakika na kuongeza kipato chao.

Akizungumza na Vijana hao mara baada ya ukaguzi wa mradi huo,Ndg. Kaim amewapongeza vijana hao kwa kuanzisha kiwanda kidogo cha kuzalisha chaki na kujihakikishia ajira na fedha iliyotolewa na Serikali inaonekana na kuiagiza Halmashauri ya Mji Makambako kuwatafutia soko la uhakika vijana hao ili wauze bidhaa zao kwa bei nzuri na kukuza kiwanda chao.

Kikundi hicho kilipata mkopo wa Mil.17.2 ambazo zilitumika kununua mashine 1 ya kutengenezea chaki yenye pleti mbili kwa gharama ya mil. 7 yenye uwezo wa kuzalisha katoni 20 zenye chaki 60,000 kwa siku ambazo wanaziuza kwenye Taasisi mbalimbali za Elimu na Maduka ya vifaa vya ofisi na kiasi kingine cha fedha kimetumika kununua malighafi,vifungashio na mashine ya EFD pamoja na uendeshaji wa kiwanda.

Kikundi cha Youth Forum ni kikundi cha Vijana wajasiriamali kilichoanzishwa rasmi mwaka 2021, kinachopatikana katika Mtaa wa Lumumba, Kata ya Mwembetogwa na kina jumla ya wanakikundi 9 ,Wanaume 8 na Mwanamke.

# MATUKIO KATIKA PICHA



**Ndg. Abdalla Shaibu Kaimu,Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,mara baada ya kukagua muendelezo wa uhifadhi wa msitu wa asili-Shule ya Sekondari Mtimbwe,**



**Ndg. Abdalla Shaibu Kaimu,Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,akikabidhi miznga 20 ya nyuki kwa wanafunzi- Sekondari ya Mtimbwe.**



**Ndg. Abdalla Shaibu Kaimu,Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,akitizama Makala ya mradi wa kilimo -wakulima walionufaika na mbolea za ruzuku katika Halmashauri ya Mji Makambako,Kulia ni Mhe. Kissa Gwakisa Kasongwa ,Mkuu wa Wilaya ya Njombe na Kushoto ni Mkulima Bi. Edda Sanga.**



**Ndg. Abdalla Shaibu Kaimu,Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,akihutubia wananchi katika mradi wa shamba la Bi, Edda Sanga,ambaye ni mmoja kati ya wakulima walionufaika na mbolea zaruzuku msimu wa mwaka huu.**

Baadhi ya mitambo na chaki zinazozalishwa katika Kiwanda cha chaki cha vijana wanufaika wa mkopo wa 10%  - Youth Forum





Mhe. Deo K. Sanga(Mb) akipanda mti wa parachichi -S/M Mawande.



Mhe. J. N. Sanga,Mwenyekiti CCM (W)Njombe akipanda mti wa parachihi- s/m Mawande.





Mhe. Kissa G. Kasongwa,Mkuu wa Wilaya ya Njombe akipanda mti wa parachichi Zahanati ya Kijiji cha Ikelu.



Jiwe la msingi la klabu ya kupinga rushwa Sekondari ya Makambako.



Nd. Kaim,Kiongozi wa mmbio za Mwenge Kitaifa akikabidhi neti kwa kina mama wajawazito na watoto.



Wanachama wa klabu ya kupinga rushwa shule ya sekondari Makambako.

# "MWENGE WA UHURU 2023"



**Baadhi ya picha za Makabidhiano ya Mwenge wa Uhuru Kati ya Mkoa wa Njombe na Iringa Kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Njombe,Mhe. Anthony Mtaka akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Iringa Mwenge wa Uhuru Tarehe 1.5.2023 viwanja vya shule ya Itandula**







*Jarida hili limeandaliwa na;*
*Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*
*Halmashauri ya Mji Makambako*
*| 19th May,2023*

*www.makambakotc.go.tz*